

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

BARUA ZOTE ZIANDIKWE KWA MKURUGENZI WA MANISPAA

SIMU: MKURUGENZI WA MANISPAA

+ 255 736 200910

OFISI ZOTE: +255 736 200911/12

FAX: +255 028 736 200910

E-mail: \*

IlemelaMunicipal@yahoo.com



Ofisi ya Mkurugenzi,  
Manispaa ya Ilemela,  
S.L.P 735,  
**MWANZA.**

Tarehe: 21 Septemba, 2016.

---

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MNAMO TAREHE 15 SEPTEMBER, 2016 GAZETI LA MWANANCHI LINALOCHAPISHWA NA KAMPUNI YA MWANANCHI COMMUNICATION LTD LILICHAPISHA HABARI YENYE KICHWA CHA HABARI **“WAPINGA KULAZIMISHWA KUSOMA ILANI YA CCM”** KUPITIA MWANDISHI WAKE NDUGU **JUMA NG’OKO.**

HABARI HIYO ILITOKANA NA KIKAO KILICHOFANYIKA SIKU YA TAREHE **19 AGOSTI 2016** AMBAPO MKUU WA WILAYA YA ILEMELA ALIKUWA AKITOA MAAGIZO MBALIMBALI KWA WAKUU WA IDARA NA WATUMISHI WA OFISI YA MANISPAA YA ILEMELA MAKAO MAKUU. KIKAO HICHO KILIHUJURIWA NA WAANDISHI WA HABARI AKIWEMO NDUGU JUMA NG’OKO.

NDUGU JUMA NG’OKO ALIENDA MBALI KWA KUSEMA KUWA ALIWAHOJI BAADHI YA WAKUU WA IDARA NA WALIDAI KUWA AGIZO LA MHESHIMIWA MKUU WA WILAYA LA KUWATAKA KUSOMA NA KUIELEWA ILANI YA UCHAGUZI YA MWAKA 2015-2020

LINAKIUKA KATIBA YA NCHI KUHUSU HAKI YA MTU KUCHAGUA CHAMA AKITAKACHO.

SOTE TUNAFHAMU KWAMBA MTUMISHI YOYOTE WA SERIKALI ILI KUWEZA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAKE KWA UFANISI HANA BUDI KUIFAHAMU NA KUIELEWA ILANI YA CHAMA KILICHOPO MADARAKANI, KWA VILE MPANGO WA BAJETI ZA HALMASHAURI NA TAIFA KWA UJUMLA HUZINGATIA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI AMBAYO NI ILANI YA CHAMA TAWALA AMBACHO NI CHAMA CHA MAPINDUZI CHENYE ILANI YA UCHAGUZI YA MWAKA 2015-2020

MKURUGENZI PAMOJA NA TIMU YA WAKUU WA IDARA WA MANISPAA YA ILEMELA WAMESIKITISHWA NA KITENDO CHA MWANDISHI HUYO **JUMA NG'OKO** KUCHAPISHA HABARI INAYOONYESHA KUWA WAKUU WA IDARA WANAPINGANA NA AGIZO LA MKUU WA WILAYA YA ILEMELA YA KUTEKELEZA ILANI HIYO.

KWA KAULI YA PAMOJA WAKUU WA IDARA WANAKANUSHA KUWA HAKUNA MKUU WA IDARA YOYOTE ALIYEHojiwa NA NDUGU JUMA NG'OKO NA KUTAMKA KAULI ZA KUWA **HAWATAKI KULAZIMISHWA KUSOMA NA KUIELEWA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2015-2020.**

**HIVYO KAULI HIZO NI ZA UONGO NA UZUSHI ZENYE NIA YA KUWACHONGANISHA WATUMISHI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA NA SERIKALI YAO.**

  
JOHN P. WANGA

MKURUGENZI

**MANISPAA YA ILEMELA**